# DARUBINI

# Sekta ya Uziduaji na Upatikanaji wa Suluhisho: Changamoto Za Watoa Msaada wa Kisheria Nchini Tanzania




Toleo 3
Disemba 2023

Imedhaminiwa na: Belgium partner in development

Imechapishwa na:
International Peace Information Services (IPIS), HakiRasilimali
Business Human Rights Tanzania (BHRT) & Avocats Sans Frontières (ASF)

Tanzania inajulikana kama taifa lenye utajiri mkubwa wa maliasili, hasa katika sekta ya ya uziduaji. Ahadi ya ustawi wa kiuchumi, imeunganishwa dhidi ya ukweli dhahiri wa mapambano juu ya kupata suluhu hasa pale shughuli za uchimbaji wa rasilimali zinapoleta madhara kwa watu au mazingira. Kwa jamii zilizoathiriwa moja kwa moja na shughuli za uziduaji, kutafuta haki kunaweza kuhisiwa kama ni changamoto isiyoweza kutatuliwa. Makala hii inaangazia matatizo yanayowakabili Watoa Msaada wa Kisheria nchini Tanzania wanapopitia sheria na sera tata zinazo ongoza na kutawala sekta ya uziduaji, kwa lengo la kutoa misaada ya kisheria kwa waathiriwa wa sekta ya uziduaji.

Tarehe 12 Mei 2021, Petra Diamonds Ltd, iliyokuwa kampuni kubwa ya Williamson Diamonds, ilikubali kulipa shilingi za kiTanzania bilioni 12.5 (takriban Euro milioni 4.7) kwa raia sabini na moja (71) wa Tanzania, waliokuwa wamewasilisha malalamiko yao katika Mahakama Kuu ya London. kwa makosa ya jinai ya kushambulia, mauaji, na kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria katika muktadha wa shughuli za kampuni[1]. Wadai 25 zaidi walijiunga na kesi hiyo baadaye, na kufanya idadi ya waathirika waliolipwa fidia kuwa 86.

[1] Petra Diamonds yafikia suluhu na wadai 71 kwa madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu katika kampuni yake tanzu ya Tanzania; inajumuisha taarifa za RAID & Leigh Day - Kituo cha Rasilimali za Biashara na Haki za Kibinadamu (business-humanrights.org)

Kesi hii mara nyingi hutajwa kuwa mfano mzuri wa kesi, kutokana na suluhu iliyofikiwa pamoja na fidia kwa upande wa walalamikaji. Ijapokuwa, kesi zinazotangazwa sana mbele ya mahakama za kigeni zinachangia katika kuleta haki kwa watu walioathiriwa na uwepo wa sekta ya uziduaji, lakini sehemu kubwa isiyo onekana, ya upatikanaji wa haki inafanywa na watoa msaada wa kisheria.

Sheria ya Msaada wa Kisheria Tanzania (2017) inasema watu wasiojiweza wana haki ya kupata msaada wa kisheria kutoka kwa watoa msaada wa kisheria. Kwa hivyo, watoa msaada wa kisheria wana jukumu muhimu katika kusaidia wanajamii walioathirika ambao hawawezi kumudu uwakilishi rasmi wa kisheria katika kutafuta haki kwa ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji unaohusishwa na uwepo wa kampuni binafsi. Vilevile watoa msaada wa kisheria wanaweza kuchangia katika kutoa suluhu kwa watu binafsi au jamii ambazo haki zao zimekiukwa. Kanuni na miongozo kutoka Umoja wa Mataifa hutoa "mchanganyiko mzuri" wa taratibu ambazo huleta suluhu kutokana na ukiukaji wa haki za binadamu tena kwa sababu ya shughuli za biashara: Miongoni mwa taratibu hizo ni pamoja na mifumo ya mahakama ya serikali, mifumo ya malalamiko isiyo ya kimahakama na mifumo isiyo ya serikali ambayo imetolewa na wafanyabiashara wenyewe[1]. Kuna uhitaji mkubwa wa usaidizi wa kisheria katika kesi hizi na swala hili haliwezi kupingwa, lakini mara nyingi watoa msaada wa kisheria lazima waweze kuongoza na kutafsiri mifumo tata na tofauti ya kisheria ili kuwasaidia waathirika kufikia njia hizi tofauti za kupata Suluhisho.

[1] https://www.ohchr.org/sites/default/files/Documents/Issues/Business/UNWG_NAPGuidance.pdf

watoa msaada wa kisheria nchini Tanzania wanakabiliwa na maelfu ya changamoto wakati wa kutafuta haki kupitia mifumo ya mahakama. watoa msaada wa kisheria mara nyingi ni mashirika madogo ya wasaidizi wa kisheria yanayo akisiwa na rasilimali chache na uwezo mdogo wa kusaidia jamii kikamilifu katika kupata suluhu. Mahitaji ya uwakilishi wa kisheria mara nyingi huwa ni makubwa kulinganisha na nguvu kazi iliyopo na msaada wa kifedha unaopatikana, jambo linalo pelekea kuwaacha bila muongozo unaofaa watu wengi walioathirika. watoa msaada wa kisheria wanakabiliwa na vikwazo katika uwezo wao wa kupeleka kesi mahakamani, kwani wanakosa nyenzo za kuwawakilisha wateja. Baadhi ya watoa msaada wa kisheria wa Tanzania wanaoweza kutafuta suluhu kupitia mfumo wa mahakama ni wale wenye uhusiano mkubwa na mashirika au miungano ya haki za binadamu, kama vile Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) au Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), ambao wanaweza kusaidia. katika kuwabakiza mawakili.

## Njia zisizo za mahakama: Ukosefu wa uaminifu

Taratibu mbalimbali zisizo za kimahakama zimeanzishwa nchini Tanzania ili kushughulikia kwa ufanisi malalamiko yanayotokana na uwepo wa shughuli za sekta ya Uziduaji. Nchi inajivunia mifumo kadhaa ya serikali isiyo ya mahakama, kama vile taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu yenye daraja "A", Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), au Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), chombo cha serikali kilichopewa mamlaka ya kutekeleza viwango vya mazingira kwa kufuatilia na kutathmini athari za mazingira za shughuli za uziduaji.

Licha ya njia hizi zinazopatikana, mradi wa utafiti uliofanywa na asasi ya kiraia Avocats Sans Frontières (ASF), unatoa mwanga juu ya mifumo hii ya utoaji misaada ya kisheria katika sekta ya Uziduaji Tanzania.

watoa msaada wa kisheria walioshiriki katika utafiti walionesha mashaka makubwa, hasa kuhusu mfumo wa kidijitali wa CHRAGG, ambao waliona "unaingilia" kutokana na mahitaji yake ya taarifa binafsi za kina wakati wa kusajili malalamiko[1]. Hofu ya kufichuliwa na athari zinazoweza kutokea kutoka kwa mamlaka ya serikali za mitaa zilizuia watoa msaada wa kisheria kujihusisha zaidi na jukwaa hilo.

[1]https://www.chragg.go.tz/lodgecomplaints

Mtoa msaada wa kisheria mmoja anaelezea kuwa: "Nilijaribu kuwasilisha malalamiko ya haki za binadamu, lakini niliacha nilipogundua kuwa mfumo huo uliuliza habari nyingi. Niliogopa kwamba ningefichuliwa na kushughulikiwa kibinafsi." Ukosefu huu wa imani kwa taasisi unasababishwa na uelewa mdogo wa mamlaka za serikali kuhusu mapendekezo ya CHRAGG[1] na ukosefu wake wa rasilimali za kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu[2]. Hali kama hiyo ilijitokeza kuhusu NEMC, ambayo ina mamlaka ya kuadhibu kwa kutofuata Tathmini ya Athari kwa Mazingira. watoa msaada wa kisheria ambao waliisaidia jamii ya Butiama vijijini (iliyopo mkoani Mara) katika kuwasilisha malalamiko ya uchafuzi wa maji uliofanywa na mgodi wa Barrick North Mara wanasema kuwa NEMC haikufanya jitihada madhubuti kufuatilia iwapo maagizo waliyotoa dhidi ya kampuni ya uchimbaji madini yalitekelezwa. Kwa hivyo, makampuni ni vigumu kuzuiwa kukomesha makosa yao au kurekebisha madhara. Ukosefu huu wa imani katika ufanisi na uadilifu wa mifumo hii isiyo ya kimahakama unakwamisha utatuzi wa malalamiko ndani ya sekta ya uziduaji nchini Tanzania.

[1] Kesi yaKituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na vingine 135 v. Mwanasheria Mkuu wa Serikali
[2]Kesi ya Wakazi wa vijiji vya Katoma na Nyakabale wilayani Geitahttps://www.ihrb.org/uploads/reports/IHRB%2C_Ch._4_Access_to_Remedy_-_Human_Rights_in_Tanzanias_Extractive_Sector_-_Exploring_the_Terrain%2C_Dec_2016.pdf

## Taratibu za Malalamiko ya Kampuni: Mapungufu ya Kiutekelezaji

Miongoni mwa maoni ya watoa misaada ya kisheria ni kwamba makampuni yana nia ya kupitisha miongozo ya kina ya utatuzi wa malalamiko yenye utaratibu mrefu kinadharia na sio kiutendaji. Baadhi yao wameshutumu kukosekana kwa muitikio wa maofisa malalamiko wa kampuni, ambao wanahisiwa kupendezwa tu na unyanyasaji ambao ni wa wazi sana tena unaoweza kuvutia ushiriki wa mashirika ya sheria ya kimataifa au mashirika ya haki za binadamu.

Mmoja miongoni mwa watoa msaada wa kisheria kutoka Tarime ambaye alijaribu kujihusisha na utaratibu wa malalamiko wa Barrick alisema: “Kampuni ilipitisha utaratibu wa malalamiko ulioandikwa vizuri,

lakini hakuna utekelezaji madhubuti. Nilikuwa na kesi ya mteja na niliomba nafasi ya kikao pamoja nao, lakini maofisa wa malalamiko waliendelea kukwepa kila siku.” Kutokuwepo kwa muitikio na uzingatiaji, aidha katika muktadha wa maombi ya taarifa au malalamiko, kumewalazimu baadhi ya watoa msaada wa kisheria kupendelea taratibu za muda mrefu za kisheria ndani ya mfumo wa mahakama.

Aidha, watoa msaada wa kisheria na walalamikaji wao wanakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo kuwepo na vitendo vya vitisho na kulipizwa kisasi na polisi wanapotaka kufuatilia kesi nyeti. Jambo linalotatiza zaidi ni kuwa miongoni mwa kampuni huorodhesha huduma za polisi kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa eneo lao, pamoja na kuingia mikataba na kampuni binafsi za ulinzi.

Jambo hili huleta ugumu haswa katika utolewaji wa taarifa kwa vyombo vya kutekeleza sheria kwa ngazi ya serikali za mtaa. Kwa hivyo, mazingira haya yasiyopendeza huongeza ugumu kwa watoa msaada wa kisheria na hukumbwa na vikwazo vikubwa katika kutafuta haki kwa wale wanaowawakilisha.



Watoa misaada ya kisheria wanakabiliwa na matatizo mengi, yapo matatizo ya ndani mfano uhaba wa rasilimali za kifedha, watu na ujuzi, vilevile na changamoto za nje na za kimuundo. Ili kuimarisha ufanyaji kazi wa watoa misaada ya kisheria, msaada wa kina katika nyanja mbalimbali za kazi zao ni muhimu. Vilevile ili kuimarisha ufanisi wao, na waweze kufaidika kwa kiasi kikubwa kunahitajika ushirikiano mzuri na thabiti pamoja na mawakili kuwezesha rufaa za kesi.

Zaidi ya hayo, mipango iliyoratibiwa ya kujenga uwezo inapaswa kuratibiwa, ikilenga kuongeza uelewa wao kuhusu utata wa kisheria ulioenea na kuinua ubora wa uwakilishi wa kisheria unaotolewa kwa jamii zilizoathiriwa.

Zaidi ya hayo, ni muhimu kwa mashirikia ya ndani na ya kimataifa kuongeza usaidizi wao katika kuwalinda watoa misaada ya kisheria. Hili linaweza kufikiwa kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo mafunzo ya kudhibiti na kupunguza hatari zinazoweza kutokea na kuimarisha ustahimilivu wa watoa misaada ya kisheria dhidi ya matatizo. Zaidi ya hayo, uwakilishi wa kisheria unapaswa kupatikana kwa urahisi wakati wowote watoa huduma hao wanapokutana na vitisho, na kuhakikisha kuwa wanaungwa mkono kukabiliana na changamoto mbalimbali za kisheria.

Kusaidia watoa misaada ya kisheria ni muhimu ili kuhakikisha kuwa jamii zilizotengwa zinapata haki na ulinzi wa kisheria. Ushirikiano kati ya watendaji mbalimbali unaweza kuimarisha uwezo wa watoa misaada ya kisheria na kuboresha uwezo wao wa kuwakilisha na kusaidia wale wanaohitaji.

## Taarifa kwa Ufupi: Taarifa kuhusu Operesheni za Kampuni ya Williamson Diamonds' na Uvunjifu wa Bwawa la Topesumu

1.Huenda Williamson Diamond akakabiliwa na Uwajibishwaji kutoka kwa NEMC kuhusu uvunjifu wa bwawa la topesumu. (Mwananchi)

2.NEMC inasisitiza kuwa Williamson atawajibika kwa fidia ya wahathirika wa uvunjifu wa bwawa la topesumu. (Mwananchi)

3.Mgodi wa Almasi wa Petra wa Williamson nchini Tanzania utaanza kufanya kazi tena mnamo Q1, 2024. (Biashara Wiz)

4.Petra Diamonds Uzalishaji Kuanza tena huko Williamson Kufuatia uvunjifu wa bwawa la topesumu. (Chanzo)

5.CHADEMA Yakataa Matokeo Kuhusu uvunjifu wa bwawa la topesumu la mgodi wa Almasi la Petra. (Chanzo)

6.Utafiti wapendekeza Hatua za kuchukuliwa na mgodi wa Almasi wa Petra ili Kurejesha Mahusiano na jamii. (Chanzo)

7.Mgodi wa Almasi Mwadui Wafidia Watu Walioathirika na Uvunjifu wa Bwawa la Mgodi. (Shinyanga Press Club)

8.Malipo ya fidia kwa wahanga wa bwawa la mgodi wa almasi ulioporomoka Mwadui yamefikia kiwango cha kuridhisha, na bwawa lililoharibika linaendelea na matengenezo. (Shinyanga Press

9.EACOP yakabidhi nyumba 339 kufidia watu walioathirika. (Habari za kila siku)

10.EACOP yakabidhi nyumba ya mwisho ya fidia. (Mwananchi)

***"Marafiki zake wawili aliokuwa nao siku hiyo ya bahati mbaya sasa wanaishi mbali, mahali fulani mkoani Simiyu. Sina namba zao za simu, hivyo sikuweza kuorodhesha taarifa hizo kwenye malalamiko niliyowasilisha kwa IGM, na sina pesa ya kuwatumia. Nimekuwa na mikutano mitatu katika ofisi ya IGM tayari. Hata nikifaulu kuwafikia marafiki hawa, sina uhakika kama bado nitapata fursa ya kuwasilisha mashahidi wapya". - Ushuhuda kutoka kwa baba ambaye aliwasilisha malalamiko kwa IGM kwa niaba ya mtoto wake, ambaye aliuawa na walinzi mnamo 2015.***



# Sauti za Jamii: Jinsi jamii zilivyo athiriwa na uchimbaji wa almasi mkoani Shinyanga na uzoefu wa juhudi za kampuni za uchimbaji madini katika kupunguza madhara

Tangu miaka ya 1940, mgodi wa almasi wa Williamson wilayani Kishapu-Tanzania, umekuwa na shughuli kubwa zaidi ya uchimbaji wa almasi. Mvutano umeongezeka kati ya mgodi na jamii za karibu, hasa kuhusu tabia za wenyeji kuingia migodini kwa ajili ya kuchunga, kukusanya kuni, au uchimbaji holela wa almasi. Ingawa mgodi huona shughuli hizi kama uvamizi haramu, wenyeji wanaziona kama njia sahihi ya kupata rasilimali muhimu kwa maisha yao.

Katika miongo kadhaa iliyopita, matukio ya wavamizi yanaonekana kuongezeka na kuzidi kuleta madhara makubwa zaidi ambayo watu wa eneo la karibu na mgodi huo wamekumbana nayo, ikiwa ni pamoja na tuhuma za kupigwa, kuteswa, kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria, kupigwa risasi ovyo, ukatili wa kijinsia na mauaji ya wakazi wa eneo hilo na walinzi binafsi wa mgodi. Hatimaye, mwaka wa 2021, madai ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu yalisababisha suluhu kubwa kati ya wadai 96 wa Kitanzania na Petra Diamonds, aliyekuwa mmiliki mkubwa wa mgodi wa Williamson.

Mwaka 2021 Petra ilianza safari ya kurejesha na kutatua changamoto katika jamii zinazozunguka mgodi wa almasi wa Williamson ikijumuisha fidia kwa waathirika, miradi ya maendeleo ya jamii na uanzishwaji wa utaratibu wa malalamiko ya kutatua changamoto ya haki za binadamu (IGM). Kulingana na ripoti mpya ya utafiti, IPIS inatathmini kuwa juhudi hizi zinaweza kuchangia kupunguza madhara, kurejesha imani kwa jamii jirani na kuhakikisha hali nzuri ya kufikia utatuzi wa changamoto. Jambo la msingi katika uchambuzi wa ripoti hii ni swali kuhusu jinsi juhudi hizi zinavyoshughulikiwa kuzingatia watu na jamii zilizoathiriwa.

Ingawa utafiti unahitimisha kuwa hatua muhimu zinachukuliwa ili kurejesha na kujenga upya mahusiano ya jamii na kuanzisha ushughulikiaji wa manung'uniko wenye maana, pia unatoa mifano mingi ya jinsi, kwa nini na wapi jamii hupata mapungufu. Mara nyingi, mapungufu haya yanaonekana kuwa yanatokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha wa kampuni ya uchimbaji madini kuhusu muktadha wa eneo hilo, hali halisi na mahitaji ya wakazi. Kwa sababu hiyo, mipango inayoanzishwa inaonekana isiyo ya kweli, isiyo na usawa na ni mipango hasi kwa wanaopaswa kufaidika nayo. Mipango fulani kufikia sasa inaonekana kuwa bora kwenye karatasi kuliko ilivyo katika utendaji, kutokana na kukosekana kwa miundo bora ya kushirikiana na jamii, na kushauriana nao kuhusu masuala yanayowahusu.

Mfano halisi ni ushuhuda wa "Rose" (sio jina lake halisi). Mwaka 2014, Rose alikwenda kumtembelea mtoto wa mdogo wake katika hospitali ya Mwadui, iliyopo eneo la leseni ya Williamson. Ili kufika nyumbani kwake katika kijiji cha Ikonongo mara baada ya giza kuingia baada ya ziara hiyo, Rose aliamua kupita njia ya mkato na baiskeli yake kuvuka eneo la mgodi. Anasema kuwa, alipokuwa akitoka nje ya eneo la mgodi, alikutana na walinzi binafsi, mmoja wao alimwambia kwamba angemruhusu aende nyumbani salama ikiwa tu atafanya naye ngono. Baada ya kukataa, anasema alianza kumpiga na kumbaka kwa nguvu. Baada ya tukio hilo, Rose alieleza, alisita kumwambia mumewe, kwa sababu aliogopa kwamba angemlaumu na kumnyanyasa.



©IPIS

***"Sina maelezo na taarifa kutoka kwa IGM. Sipati majibu kutoka kwao ili kunisaidia kuelewa kama nina ushahidi unaofaa na wa kutosha kwa malalamiko yangu" – Malalamiko kutoka kwa anayedaiwa kuwa muathirika wa kupigwa na walinzi binafsi wa mgodi huo.***

Pia hakumuona daktari bali alitumia tu dawa za kutuliza maumivu ili kumaliza siku baada ya dhuluma hiyo. Mume wake alipojua kilichotokea, aliichukulia taarifa hiyo vibaya, akamlaumu, akampiga na hatimaye kumuacha Rose na watoto wao watano.

Mnamo mwaka wa 2021, Rose alisikia kuhusu kitengo binafsi cha malalamiko cha Williamson (IGM) na akaenda kwenye ofisi ya mahusiano ya jamii ya mgodi ili kuwasilisha malalamiko. Aliambiwa kwamba ofisi haikuwa ikichukua malalamiko yoyote kwa wakati huo, lakini mtu kutoka IGM atampigia simu watakapofungua usajili. Rose hakupokea simu kama hizo lakini alisikia kutoka kwa wanakijiji wengine, mnamo Juni 2022, kwamba ofisi ilikuwa ikisajili tena malalamiko. Muda mfupi baadaye, Rose alifanikiwa kuandikisha malalamiko yake. Hata hivyo, hakuweza kuorodhesha mashahidi wowote: kwamaana alikuwa peke yake wakati unyanyasaji ulipotokea, wanafamilia ambao walikuwa naye baada ya matokeo hawakuweza tena kutoa ushahidi. Baba yake alikuwa amefariki na dadake mdogo sasa anaishi umbali wa kilomita 500.

Mnamo Februari 2023, aliitwa kwa mahojiano yake ya kwanza. Mnamo Aprili 2023 alipigiwa simu ya pili, ikimuagiza kufika katika ofisi ya IGM Shinyanga mjini. Aliambiwa asafiri hadi ofisini kwa gharama zake mwenyewe, kwani gari la IGM lilikuwa tayari limepita mara kadhaa kijijini kwake, na timu ya IGM haikuweza kumfikia. Kwenye mazungumzo ya simu

Afisa wa IGM alisema alete mashahidi wake, jambo ambalo alieleza kuwa haliwezekani kwake. Mwishowe, alienda kwenye mahojiano ya pili peke yake, na kisha akaambiwa asubiri simu nyingine. Rose anasema amekuwa akingojea simu hiyo tangu wakati huo. Unaweza kusoma ushuhuda kamili wa Rose na ushuhuda mwingine wa jamii katika ripoti ya IPIS"Jaribio la Petra Diamonds kujisafisha na historia yake chafu nchini Tanzania. Changamoto katika upatikanaji wa suluhu na kurejesha mahusiano na jamii baada ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika mgodi wa almasi wa Williamson.."

Kama sehemu ya mikakati yao mipya ya kushughulikia malalamiko, Petra na Williamson Diamonds wanaonesha kuwa wamejitolea kujifunza na kuboresha wakati wanaendelea kutekeleza usuluhishi na kurejesha uhusiano mzuri kwa jamii inayozunguka mgodi wa almasi wa Williamson. Kufanya hivyo kwa ushirikiano wa kweli na jamii itakuwa muhimu ili kuondokana na mapungufu ya awali, kurejesha uaminifu na kujenga mahusiano mazuri ya muda mrefu ya jamii.

***"Nilipowaeleza maofisa wa IGM kuhusu walinzi hao walichonifanyia mwaka 2017 baadhi yao walinijibu kuwa ninadanganya, kwamba mimi ni mhalifu niliyeingia mgodini kinyume cha sheria na walinzi hawakufanya kosa lolote. Iliniuma sana kusikia hivyo, kwani nilikuwa na matumaini ya kupata kutambuliwa" - Ushuhuda kutoka kwa kijana wa kijiji cha Songwa ambaye aliwasilisha madai kwa IGM kuhusiana na jeraha kubwa la mguu kufuatia kupigwa na walinzi wa mgodi huo.***

IPIS · HakiRasilimali – Enhancing Transparency & Accountability of the Extractive Industry in Tanzania · BHRT – Business and Human Rights Tanzania · Avocats Sans Frontières